

BODI YA PAMBA TANZANIA



**MWONGOZO NA. 1 WA MSIMU WA 2023/2024 KUHUSU
MFUMO WA USIMAMIZI NA UUZAJI WA PAMBA
ULIOTOLEWA KWA SHERIA YA TASNIA YA PAMBA NA. 2
YA MWAKA 2001 NA KANUNI ZA TASNIA YA PAMBA ZA
MWAKA 2011**

(Simiyu Model)

**Umetayarishwa na: -
Bodi ya Pamba Tanzania,
S. L. P. 61,
MWANZA.**

**Simu : (028) 2500528.
Barua pepe : info@tcb.go.tz
Tovuti : www.tcb.go.tz**

29 MEI, 2023

UTANGULIZI

Uzalishaji na uuzaji wa pamba nchini Tanzania unasimamiwa na Sheria ya Tasnia ya Pamba Na. 2 ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2011. Sheria na Kanuni zinaweka masharti ya msingi kwa ajili ya kuzingatiwa na mzalishaji, mnunuzi na muuzaji wa pamba ndani na nje ya nchi, pamoja na wadau wengine wa pamba ili kuhakikisha kuwa pamba inayozalishwa, kununuliwa na kuuzwa hapa nchini na nje ya nchi inakidhi ubora unaokubalika kimataifa ili kuiwezesha kupata soko la uhakika. Sheria pia inalenga kumhakikishia mtumiaji wa bidhaa za pamba kupata bidhaa zenye ubora wa uhakika.

Mwongozo huu unatambulika kama “Mwongozo Na. 1 wa Mwaka 2023 Mfumo wa Simiyu” unaoelekeza taratibu za usimamizi na uuzaji wa pamba ambao umeandaliwa kwa mujibu wa **Kanuni ya 45** ya Kanuni za Tasnia ya Pamba za Mwaka 2011.

Utaratibu huu utatumika katika wilaya zote za mkoa wa Simiyu, pamoja na wilaya za Magu na Kwimba mkoani Mwanza. Mwongozo huu unatoa maelekezo ya jumla kwa wadau wote wa Tasnia ya Pamba nchini kuhusu utaratibu wa ununuzi wa pamba katika maeneo yaliyoainishwa ambapo kampuni binafsi zitakuwa na vituo binafsi vya kununulia pamba na Vyama Vikuu vya Ushirika vitanunua kupitia AMCOS zake.

Aidha, unaweka na kufafanua utaratibu mzima wa mfumo wa usimamizi na uuzaji wa pamba na masharti ya msingi yaliyomo katika Sheria na Kanuni za Pamba. Utaratibu huo ni kuhusu uuzaji wa pamba, malipo kwa wakulima, usafirishaji wa pamba hadi kiwanda cha kuchambua pamba na wajibu wa kila mdau katika kutekeleza maelekezo ya Serikali kuwa wakulima wauze pamba katika vituo vilivyoidhinishwa na Bodi ya Pamba.

SEHEMU YA KWANZA
TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo: -

AMCOS Chama cha Ushirika cha Msingi kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na kinachojihusisha na Kilimo na Masoko.

CCN Hati ya kupokelea pamba viwandani.

CDTF Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Pamba.

DPN Daily Purchasing Note

Ghala **Jengo lililoidhinishwa** kupokea na kuhifadha pamba.

Kituo cha Kununulia Pamba: Sehemu iliyoidhinishwa mahsusi kwa ajili ya kuuzia na kununulia pamba kutoka kwa wakulima.

Mnunuzi Kampuni iliyoidhinishwa na Bodi ya Pamba Tanzania kununua na kuchambua pamba katika eneo lililoainishwa katika msimu husika.

Kikosi Kazi cha Wilaya: Kamati inayoundwa na Watumishi wa Serikali katika ngazi ya Wilaya kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi wa mauzo ya pamba.

Mkaguzi wa Ubona: Mtumishi wa umma mwenye taaluma ya ubora wa pamba aliyeidhinishwa kukagua pamba iliyopo kwenye kituo cha kununulia pamba, ghala, gari, shamba, kiwanda cha kuchambua pamba na mahali pengine popote ambapo panahusika na pamba.

Sheria Sheria ya Tasnia ya Pamba Na. 2 ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2009.

TCB Bodi ya Pamba Tanzania
TCDC Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania.
UNION Chama Kikuu cha Ushirika kilichosajiliwa chini ya Sheria
ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013
kinachojihusisha na Kilimo na Masoko ya mazao.

SEHEMU YA PILI

USIMAMIZI WA TASNIA YA PAMBA TANZANIA

2.1 Sheria na Kanuni za Tasia ya Pamba

Tasia ya Pamba nchini inaongozwa na kusimamiwa na Sheria ya Tasia ya Pamba Na. 2 ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2009, na Kanuni zake za Mwaka 2011.

2.2 Bodi ya Pamba Tanzania

Sheria ya Tasia ya Pamba Na. 2 ya Mwaka 2001, inaipa Bodi ya Pamba Tanzania mamlaka ya kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu Tasia ya Pamba nchini.

SEHEMU YA TATU

UNUNUZI NA UUZAJI WA PAMBA

- 3.1 Simiyu "Model" itatumika kwa wilaya zote za mkoa wa Simiyu pamoja na wilaya za Kwimba na Magu za mkoa wa Mwanza.
- 3.2 Pamba itauzwa na kununuliwa katika vituo vya kampuni binafsi ama kwa kampuni zitakazopenda, zinaweza kutumia Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) vitakavyoidhinishwa na Bodi ya Pamba. Ikiwa kampuni itaamua kutumia AMCOS, haitaruhusiwa kufungua kituo binafsi katika kijiji hicho.
- 3.3 Utaratibu wa ununuzi wa pamba hai (Organic Cotton) utakuwa kama ifuatavyo;
 - a) Kila kampuni inayozalisha pamba hai ni lazima iwe na ghala maalum kwa ajili ya pamba hai katika kila kijiji inakozalisha pamba hiyo. Haitaruhusiwa ghala moja kutumika kwa pamba ya kawaida na pamba hai kwa namna yoyote, ile.
 - b) Orodha ya wakulima wa kila kampuni katika Eneo husika na taarifa zao ni lazima yabandikwe katika kila ghala lililotengwa kwa ajili ya kununulia pamba hai;
 - c) Stakabadhi za mazao na nyaraka nyingine za mauzo kwa ajili ya pamba hai hazitaruhusiwa kuchanganywa na zile zinazotumika kwa pamba ya kawaida;
 - d) Taarifa za manunuzi ya pamba ni lazima zijazwe kwenye 'ledger' maalum inayotolewa na Bodi ya Pamba;
 - e) Ni lazima kila kampuni ibandike bango la bei yake katika ghala la kununulia pamba katika eneo linaloonekana kwa urahisi na bei hiyo ni lazima iwe juu ya bei ya pamba ya kawaida iliyoko sokoni kwa wakati huo;

- f) Kumbukumbu zote za mauzo zitakuwa zinafanyiwa Ukaguzi wa mara kwa mara na maafisa kutoka Bodi ya Pamba kadri itakavyoonekana inafaa;
 - g) Kampuni yoyote itakayobainika kununua pamba ya kawaida na kuitafsiri kama pamba hai, itafutiwa leseni yake ya ununuzi mara moja
- 3.4 Wanunuzi wa Pamba watakuwa kampuni binafsi na Vyama Vikuu vya Ushirika.
- 3.5 Kwa hiari ya mkulima mwenyewe, malipo kwa pamba aliyouza yatafanyika kupitia moja kati ya njia zifuatazo.
- i. Fedha taslimu katika kituo cha ununuzi punde uhakiki wa ubora na upimaji wa pamba ya mkulima unapokamilika.
 - ii. Akaunti za benki au simu za mkononi. Malipo yafanyike ndani ya saa 48 baada ya pamba ya mkulima kupokelewa kwenye kiwanda cha pamba.
- 3.6 Bodi ya Pamba itatoa leseni za ununuzi wa pamba kwa kampuni binafsi na Vyama Vikuu vya Ushirika.
- 3.7 Mizani ya digitali na ya saa iliyohakikiwa na kupasishwa na Wakala wa Vipimo ndiyo pekee itakayotumika kupima pamba ya mkulima.
- 3.8 Mkulima atapewa risiti inayoonesha uzito, bei na thamani ya pamba aliyouza na wakati wa malipo atalipwa kulingana na bei na thamani iliyoandikwa katika risiti.
- 3.9 Kila mnunuzi atakuwa na bango lenye kuonesha bei yake kwa kila siku katika kituo cha ununuzi ambayo haitakuwa chini ya bei dira.
- 3.10 Ili kuongeza uwazi wa bei katika vituo vya ununuzi, kila kituo cha ununuzi kitakuwa na “ledger” itakayoandaliwa na Bodi ya Pamba. Ledger hii itakuwa inajazwa na kusainiwa na Afisa Shughuli wa

Kampuni pamoja na karani wa kituo ikionesha mabadiliko ya bei na muda wa mabadiliko yalipofanyika na itakuwa ikikaguliwa na mamlaka za serikali wakati wowote ikihitajika.

- 3.11 Kampuni binafsi zinahiari ya kutumia Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) kama wakala wa ununuzi wa Pamba.
- 3.12 Ikiwa kampuni itachagua kutumia AMCOS kama wakala wa ununuzi, vitabu vya kampuni vya stakabadhi ya mazao na vitabu vingine ndivyo vitakavyotumika katika miamala yote.
- 3.13 Madeni ya pembejeo kwa msimu wa kilimo wa 2022/23 hayatakatwa kutoka kwa mkulima wakati wa kuuza pamba yake.

SEHEMU YA NNE
WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI WA TASNIA YA
PAMBA

4.1 BODI YA PAMBA TANZANIA (TCB)

- i. Kutoa leseni za ununuzi na uchambuaaji wa pamba kwa kampuni binafsi na Vyama Vikuu vya Ushirika;
- ii. Kuratibu na kutoa Mwongozo wa Serikali kuhusu usimamizi na uuzaji wa zao la pamba;
- iii. Kusimamia, kukagua na kutoa elimu kuhusu usafi na ubora wa pamba katika ngazi zote;
- iv. Kutangaza bei dira ya pamba kwa mkulima kabla ya kufungua msimu;
- v. Kufuatilia mwenendo wa bei ya pamba katika soko la dunia na kuratibu marejeo ya bei dira pale inapobidi.
- vi. Kusimamia na kuhakikisha pamba ya wakulima iliyopelekwa na kuuzwa katika vituo vya ununuzi inalipwa kabla ya kusafirishwa kwenda kiwandani;
- vii. Kutekeleza majukumu mengine kadri yatakavyokuwa yakijitokeza kwa kushirikiana na wadau wengine wa utekelezaji.
- viii. Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mwenendo wa hali ya soko la pamba duniani.
- ix. Kuandaa “ledger” kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenendo wa mabadiliko ya bei na kuzisambaza kwenye vituo vya ununuzi.
- x. Kutatua Migogoro inayojitokeza katika uuzaji na ununuzi

4.2 TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)

- i. Kutoa maelekezo ya kiwango cha gharama cha kuzingatiwa na AMCOS katika kugharamia posho ya mjumbe atakayesimamia ununuzi wa pamba katika kituo cha ununuzi cha AMCOS ili kuepusha matumizi yasiyokuwa ya lazima;
- ii. Kusimamia Mwenendo mzima wa shughuli za AMCOS kwa kipindi chote cha ununuzi wa pamba ili kubaini mapungufu na kuchukua hatua stahiki mapema.
- iii. Kutoa Waraka wa Mrajis ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo ya mgawanyo wa gharama za ununuzi wa pamba miongoni mwa AMCOS, UNION na TCDC kwa AMCOS ambazo zitazininulia kampuni binafsi.
- iv. Kuhamasisha na kuhakikisha AMCOS na wakulima wote wa pamba wanafungua akaunti benki.
- v. Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mwenendo wa hali ya soko la pamba duniani.

4.3 TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)

4.3.1 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

- i. Kuhakikisha kuwa pamba yote inanunuliwa kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali;
- ii. Kuratibu na kusimamia shughuli za Vikosi Kazi katika ngazi zote kuhusiana na ununuzi wa pamba.
- iii. Kupitia na kutoa mapendekezo juu ya maombi ya wanunuzi wa pamba kwa msimu husika kwa Bodi ya

Pamba kwa wakati ili leseni za ununuzi ziweze kutolewa kwa wakati;

4.3.2 Ofisi ya Mkuu Wa Wilaya

- i. Kuhakikisha kuwa pamba yote inanunuliwa kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali;
- ii. Kuhakikisha Kikosi Kazi kinatekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa mujibu wa sheria;
- iii. Kuhakikisha maombi ya wanunuzi wa pamba mbegu yaliyowasilishwa yanashughulikiwa kwa wakati;

4.3.3 Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa na Jiji

- i. Kuwaruhusu wanunuzi wa pamba katika maeneo yao kuingia na kununua pamba mahali popote wanapotaka ili kuleta ushindani;
- ii. Kutambua na kuidhinisha vitabu vya stakabadhi za mazao zitakazotumika kwenye vituo vya ununuzi pamoja na nyaraka nyingine za ununuzi wa pamba;
- iii. Kusimamia utendaji wa AMCOS wakati wa ununuzi wa pamba kwa mujibu wa sheria;
- iv. Kusimamia na kuhakikisha kuwa vibali vya kusafirisha pamba kutoka vituoni kwenda viwandani vinatolewa kwa wakati pasipo kuchelewesha usafirishaji;
- v. Kuhakikisha kampuni zinazonunua pamba zinatoa taarifa sahihi za ununuzi kila wiki;
- vi. Kuhamasisha wakulima kufungua akaunti benki;

- vii. Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mfumo wa malipo ya mauzo yao ya pamba kupitia akaunti zao za benki au simu za mkononi;
- viii. Kuhakikisha biashara ya pamba kwenye maeneo yao inafanyika kwa kuzingatia sheria;
- ix. Kusimamia na kuhakikisha kuwa kampuni/Union zimewalipa wakulima fedha za mauzo yao ya pamba pale ambapo malipo yanafanyika kwa fedha taslimu.
- x. Kutoruhusu gari la kampuni kuchukua pamba ya wakulima ikiwa deni la pamba iliyochukuliwa mwanzoni na kampuni hiyo katika kituo husika halijalipwa.

4.4 WAKALA WA VIPIMO

- i. Kukagua na kuthibitisha mizani ya kupimia pamba kabla ya msimu kuanza;
- ii. Kutoa mafunzo ya upimaji sahihi katika mizani kwa wakulima, AMCOS na makarani wa kampuni;
- iii. Kufanya ukaguzi wa mizani ya kupimia pamba vituoni na viwandani wakati msimu wa ununuzi ukiendelea;
- iv. Kutatua migogoro inayotokana na malalamiko ya utofauti wa uzito wa pamba baina ya Wakulima, wakala na kampuni;

4.5 CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA

- i. Kuandaa na kusambaza shajala za ununuzi wa pamba zitakazotumiwa na AMCOS mahali ambapo Chama Kikuu cha Ushirika kitanunua pamba.

- ii. Kuhakikisha AMCOS zote zimefungua akaunti benki zitakazotumiwa na wanunuzi kulipa fedha za gharama za ununuzi pamba;
- iii. Kutunza kwa usahihi takwimu za ununuzi wa pamba kutoka kwa wakulima na kutoa taarifa kwa mamlaka husika zikiwemo TCB, TCDC, Halmashauri ya Wilaya ya eneo husika pamoja na wadau wengine pindi inapohitajika;
- iv. Kusimamia Mwenendo mzima wa shughuli za AMCOS kwa kipindi chote cha ununuzi wa pamba ili kubaini mapungufu na kuchukua hatua stahiki mapema.
- v. Kusimamia na kutekeleza majukumu mengine ya msingi kwa kadri yatakavyokuwa yakitolewa na TCB na TCDC.

4.6 VYAMA VYA USHIRIKA VYA MSINGI (AMCOS)

- i. Kuajiri watendaji wa kutosha na wenye sifa kulingana na idadi ya vituo vitakavyotumika kununua pamba.
- ii. Kusimamia uzito wa pamba iliyonunuliwa kwenye AMCOS kwa kupima uzito wa kila gunia na kujaza katika hati maalum (tally sheet) itakayosainiwa na mtendaji wa AMCOS na wakala wa kampuni kabla ya kusafirisha pamba kwenda kiwandani.
- iii. Kutunza kwa usahihi takwimu za ununuzi wa pamba kutoka kwa wakulima na kutoa taarifa sahihi kwa wadau wa usimamizi pindi zitakapohitajika;
- iv. Kuandaa taarifa ya wiki ya pamba yote iliyonunuliwa na kusafirishwa kwenda viwandani na kuituma kwenda kwa

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na Bodi ya Pamba.

- v. Kupokea na kuhifadhi nakala ya hati ya uzito wa pamba iliyopokelewa kiwandani (CCN);
- vi. Kufungua akaunti benki kwa ajili ya malipo ya gharama za uendeshaji wa shughuli ya ununuzi wa pamba za AMCOS;
- vii. Kusimamia na kutekeleza majukumu mengine kwa kushirikiana na TCDC, UNION na TCB kadri yatakavyokuwa yakijitokeza;

4.7 WAKULIMA WA PAMBA

- i. Kuvuna pamba kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora;
- ii. Kutenga pamba katika daraja “A” na “B”; kabla ya kuipeleka katika kituo cha ununuzi;
- iii. Kutumia mifuko sahihi na inayokubalika kwa ajili ya kuvuna, kuhifadhi na kusafirisha pamba.
- iv. Kudai stakabadhi ya mazao iliyoandikwa uzito na bei halisi aliyouza siku hiyo;

4.8 WANUNUZI WA PAMBA

- i. Kuwa na leseni ya kununulia na kuchambulia pamba inayotolewa na Bodi ya Pamba.
- ii. Kuandaa ghala lenye sifa zinazokubalika kwa mujibu wa sheria ya pamba kwa ajili ya kununua na kuhifadhi pamba;
- iii. Kufukiza dawa (fumigation) kwenye maghala yote yatakayotumika kwenye ununuzi wa pamba;

- iv. Kuandaa vitabu vya stakabadhi ya mazao na kuviwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa ajili ya kutambuliwa na kuidhinishwa;
- v. Kuandaa vitabu “Daily Purchasing Note” kwa ajili ya kutolea taarifa ya kila siku kuonesha jumla ya kiasi cha pamba kilichonunuliwa kwa kila siku katika kila kituo.
- vi. Kuhakikisha kuwa nyaraka zote zinazohitajika na zinazotosheleza mahitaji ya ununuzi na usafirishaji wa pamba kwa kipindi chote cha ununuzi zimefikishwa katika kituo cha ununuzi;
- vii. Kuhakikisha kila mkulima aliyeuza pamba katika kituo husika amepatiwa stakabadhi ya mazao yenye uzito na bei halisi ya siku hiyo;
- viii. Kununua pamba kwa kuzingatia usafi na ubora wa pamba kwa kuitenga katika madaraja “A” na “B” kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Tasnia ya Pamba.
- ix. Kutoa taarifa kwa kila wiki ya ununuzi na usafirishaji wa pamba kwa TCB, Halmashauri ya Wilaya na nakala kwa Katibu Tawala wa Mkoa.
- x. Kuhakikisha kuwa “tally sheet” wakati wa kusafirisha Pamba, “ledger” wakati bei ya Pamba inapobadilika imesainiwa na wakala wa kampuni na mtendaji wa AMCOS.
- xi. Kuandaa taarifa ya kuonesha jumla ya kiasi cha pamba kilichonunuliwa kwa siku kwa kujaza “Daily Purchasing Note”.

- xii. Kulipa ushuru wa Halmashauri na Mfuko wa CDTF kama ilivyokubaliwa katika mjengeko wa bei.
- xiii. Katika gharama ya ununuzi ya shilingi 60 kwa kilo iliyokubalika kwenye mjengeko wa bei, kampuni itakayonunua kupitia AMCOS italipa gharama ya ununuzi kwa UNION, AMCOS na TCDC jumla ya shilingi 58 kwa kila kilo moja ya pamba itakayonunuliwa na shilingi 2 itabaki katika kampuni kwa ajili ya gharama za shajala.
- xiv. Kampuni itakayonunua kupitia vituo vyake binafsi haitalipa fedha yoyote kwa AMCOS, yaani shilingi 60 itatumika katika gharama za ununuzi za kampuni husika.
- xv. Kuhakikisha kuwa mabadiliko ya bei yanaandikwa kwenye risiti inayofuata baada ya risiti ya mwisho ya bei ya awali katika stakabadhi ya mazao pamoja na ledger ya mabadiliko ya bei inayoandaliwa na Bodi ya Pamba. Aidha, risiti iliyoandikwa mabadiliko ya bei kuonesha tarehe na muda wa kuanza kutumika kwa bei mpya, inapaswa kubaki kwenye kitabu cha stakabadhi ya mazao ikiwa ni kumbukumbu ya mabadiliko ya bei
- xvi. Kuhakikisha kwamba pamba kutoka katika AMCOS inapimwa na kushushwa ndani ya siku 2 baada ya kufikishwa kiwandani. Ikitokea ucheleweshaji wa zaidi ya masaa hayo, gharama za kujikimu za msindikizaji zitalipwa na mnunuzi kwa kiasi cha shilingi 25,000 kwa siku;

SEHEMU YA TANO

USULUHISHI WA MIGOGORO

- 5.1 Endapo kutatokea malalamiko ya upande mmoja kutotendewa haki na upande mwingine, mlalamikaji atatakiwa kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba ndani ya siku 14 tangu tarehe ya tukio.
- 5.2 Bodi ya Pamba itaitisha kikao cha usuluhishi ndani ya siku 21 tangu kupokea malalamiko kwa ajili ya kusikiliza na kutoa maelekezo ya namna ya kumaliza jambo husika kwa mujibu wa Sheria.

Hitimisho:

Mwongozo huu unatakiwa kusomwa kwa pamoja na Sheria ya Tasmania ya Pamba Na. 2 ya Mwaka, 2001 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2009 na Kanuni za Tasmania ya Pamba za mwaka 2011.

Mwongozo huu umetolewa tarehe 29 Mei, 2023.



Marco C. Mtunga
MKURUGENZI MKUU